BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

POMADE
YA MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

Hasha Si Kujiuzulu - Maulana

NAPENDA kujitokeza humu gazetini kukanusha habari iliyotolewa wiki mbili iliyopita kwamba eti nilijiuzulu kama Mwenyekiti wa Klabu ya Black Panther FC kwa ajili ya shughuli nyingi.

Nachukuwa fursa hii kuwafahamisha wananchama, wanakamati wachezaji pamoja na mashabiki wa Black Panther kwamba taarifa ya gazeti hilo la Kiingereza (sio *COASTWEEK*) haikuwa ya kweli.

Mimi ningali Mwenyekiti wa Black Panther FC na nitaendelea kushikilia usukani hadi wakati wanachama watakpoamua kuniachisha wadhifa huo. Nasema tena ningali Mwenyekiti wa Panther FC.

Napenda kuwajulisha wanachama wote kwamba Mkutano Mkuu wa Klabu ya Black Panther FC utafanyika kwenye Makao Makuu ya klabu hapo Gatundu Road siku ya Jumapili hii Mei 13 kuanzia saa nne asubuhi.

MAENDELEO

Nawaomba wanachama wote pamoja na wachezaji wasikose kufika klabu kuhudhuria mkutano huo ili tupange mipango ya maendeleo pamoja na kuchagua viongozi kwa kipindi cha 1984/85.

OMAR SHERIFF MAULANA
MOMBASA.

MENEJA MKUU wa Mvita Bottlers Limited, Bw. Salim Shirazy (mwenye miwani) akipokea zawadi bora ya 1983 kutoka kwa Mkurugenzi anayeshughulikia Bara la Africa la Kampuni ya Pepsi International, Bw. Guy Ubghs hapa mjini Mombasa.

PICHA: CAESAR MADDANGANHA

Sheikh Shirazy Awatakia Kheri Na Baraka Za Ramadhan

TAMIMU wa Thalatha Twaifa, Sheikh Mohammed Salim Shirazy ametoa wito kwa Waislamu wajitayarishe kwa ajili ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhan ambao unatarajia kuandama mwanzoni mwa Mwezi wa Juni.

Bw. Shirazy (pichani) amewatakia Waislamu popote walipo kote nchini kila la Kheri na Baraka katika kutimiza wajibu wa kufunga mwezi mzima wa Ramadhani.

Stori: Abdulrahman Sheriff

AMIHAQ ... MZEE SIMSIM JIRANI YAKE

SEHEMU YA 2

AMIHAQ alikuwa kijana yatima aliyefiwa na wazazi wake wote wawili. Vijana wenzake ama mabarobaro pamoja na "viruka njia" walijaribu kumpoteza asinyokewe na mambo yake. Sasa Enelea na msisimko huu uliotungwa na *Abdulrahman Sheriff.*

ILIMCHUKUWA muda mwingi Amihaq kupambana na vidosho pamoja na vijana wenzake ambao kila siku walikuwa wakifika nyumbani na kumshauri atoke nje, atembee nao ili aondoe mawazo mabaya ya kuwakumbuka wazazi wake. Hata hivyo, Amihaq aliwashauri waachane naye ili apate kufikiria njia nzuri ambazo zitamletea mafanikio kwenye maisha yake.

Amihaq alikuwa akiishi katika nyumba aliyoachiwa na babake na hapo jirani alikuwako mzee mwenye umri wa miaka 75 hivi aliyeitwa Simsim. Huyu Simsim alikuwa rafiki mkubwa wa babake Amihaq na kable ya Kashmun kuaga dunia, alimshika mkono Simsim na kumwomba amwangalie mwanawe sio kwa chakula ama masomo lakini kumuongoza katika njia ya mafanikio ya duniani na akhera.

Kwa kuwa Simsim naye hakuwa na mtoto ama jamaa yoyote, alimchukulia Amihaq kama mwanawe wa kumzaa na akawa kila wakati akimpa mashauri mema; mashauri ya kumwelekeza uovu na uzuri wa wanaadamu. Na kila anaposhauriwa, Amihaq aliyashika na kuyazingatia kwa makini.

Kijana akaanza kutafuta mbinu mpya za kujiendeleza kibashara. akiwa na kiasi cha 35,000/-, alionelea ni ubora amshauri Simsim juu ya kuanzisha duka la nguo badala ya kuendelea na biashara ya rejareja ya bidhaa ndogo ndogo ambayo faida yake huwa ni kiasi ama haba.

Amihq akafika nyumbani kwa Simsim na kumwambia lengo lake na akataka shauri kwake. Simsim bila ya kusita alimwambia Amihaq, "Tawak-kal mwanangu, mimi ni pamoja nawe na nakutakia kila la kheri na baraka upate kufanikiwa na lengo lako hilo ambalo ni la busara sana".

Kijana akamshukuru Simsim na kumwambia, "maadamu nimepata kibali kutoka kwako, sasa ndio ninaamua kuanza kwenda mbio ili lengu langu hili lifanikiwe. Sina shaka wewe kama mzazi wangu umeshanipa radhi, na radhi yako ndiyo itakayonisaidia". Simsim akasema: "ahsante na nenda mwanangu, lililo na kheri Mungu atakuegeshea na la shari atakwepushia".

Amihaq akaondoka moja kwa moja hadi katika Madrassa ambapo watoto walikuwa wakisomeshwa. Akatia mfukoni na kutoa 450/- akamkabidhi Mwalimu wa Madrassa hiyo. "Tafadhali Mwalimu wagawanyie wanafunzi wote pesa hizi na uwaambie waniombee Mungu mambo yangu yaniendee vizuri na hizi 100/- ni zako nawe pia unitakie kila la kheri".

Kijana Amihaq akimhudumia mnunuzi kwenye duka ... na Marehemu babake.

Akashika njia ... zake moja kwa ... afisi za Serkali ya ... ili kutafuta njia ... kufuatwa ili apate ... kuazisha biashara ... Ingawa alikuwa ... sehemu nzuri ya ... alionelea ni ... aanzie kwenye ... duka ambalo ... mzazi wake Kashmun.

Ni kweli vile walivyosema, "Palipo na Njia Ipo" hakuchukuwa muda ... akampata Afisa ... Serkali ya Ilazu ... leseni za biashara ... ambaye alimpa ... mazuri ya kutana ... biashara yake. Kijana ... leseni yake na ... kazi hiyo mara ... aliianza kwa ... lakini kila siku ... mambo yanazidi ... mema.

Je, mambo yata... mazuri kwa biashara ... zisha Amihaq ama ... utakaomfika? Na... kwa wiki hii lakini ... usikose nakili ... ufahamu yale ... fikia kijana huyo ... kuanzisha maisha ...

Farucci

BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA 'BINT EL SUDAN - GIFT PACK' KWA WASHINDI WA PILI NA WATATU KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

CROSSWORD No. 186

KWENDA KULIA: 1. Ukata, hali ya kuwa maskini kabisa. 7. Mtoto ndani yatumbo la binadamu au mnyama. 9. Uwerevu, hila. 10. Urolho, tabia ya kupenda kula sana. 15. Ala ya kisu. 16. Nemo la kuuliza swali. 18. Mwenye..... kikali ndiye alae nyama. 19. Na wewe. 21. Sumbua, hangaisha. 22. Kikalio. 23. Chukua mke.

KWENDA CHINI: 1. Aina ya nafaka. 2. Uzito. 3. Ampe habari. 4. Pesa za kizamani. 5. Wakati wa mchana. 6. Nemo la kukanusha. 8. Kibofu kikubwa. 11. Iangalie. 13. Lau, kama. 14. Elimu. 17. kama. 19. Mdudu hatari. 20. Wingi wa yeye.

Majibu ya shindano la Fumbo la Kujaza Maneno No. 185. *Kwenda Kulia:* 1. KIDARI, 5. KUTI, 6. TUNUTU, 7. LULU, 8. TIMU, 9. EA, 11. PIA, 13. NGIRI, 16. NIA, 17. LAU, 19. AE, 20. INAMA. KWENDA CHINI: 1. KITALE, 2. ASUMINI, 3. IKULU, 4. MTALII ; 10. ANIA, 12. AMUA, 14. GAE, 15. RAI, 17. LA, 18. AM.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK.

WASHINDI WA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 185.

1. Mohamed Kussema, Sanduku La posta 80149, Mombasa. 2. M. K. Kumenzwa, Sanduku La Posta 46 Kwale, Bahakanda C/O School 3. Grace I. Scyllus Sanduku La Posta Lamu Methodist 95, Lamu.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yetakayokubaliwa. Washindi watatu kila baadia yawiki mbili watapata viatu na 'Bint El Sudan - Gift Pack". Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK* limited Mombasa. Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Mihariri *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya jumatano tarehe May 16. 1984 saa, nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho.



JINA....................................

SANDUKU LA POSTA.......................

....

ASEMAVYO MHA...

UWANJA wa Manispaa ya Mombasa unatumika kwa mashindano ya hapa nyumbani pekee, bali hata mapambano ya michezo ya Kimataifa kama mechi za Challenge Cup pamoja na Klabu Bingwa za Afrika Mashariki na Kati.

UWANJA huo unastahili kuwa msafi na kutizamwa ili kila wakati uchaguliwe kama sehemu ya kufanyia mashindano ya kimataifa. Ukiwa uwanja utatizamwa ipasavyo, hakuna shaka Vyama Vya Michezo nchini utaupa nafasi ya kuchezewa mechi ama mashindano dhidi ya Mataifa mbali mbali.

JAMBO la kuhuzunisha zaidi juu ya uwanja huo ni vyoo vyake ambavyo viko katika hali ya kutoridhisha kabisa na sijui kama kuna wasimamizi wanaotizama sehemu ya kujisaidia. Ni... wakati wa ... kugombania Kla... Afrika Mashariki ...

WAKATI hu... mwenzangu wa ... kuwa akiandik... jirani ya Kenya ... kujisaidia, alin... mbaya ya vyoo ... Stadium. Na u... hali iko mba... hushindwa ku... uvundo ulioko ...

BARAZA la ... Mombasa ndilo ... la kusimamia ... haina budi ku... juu ya uchafu ... kwa vyoo hiv... uchungu, lakini ... ukweli usema... nyingine aibu ... mbali!

HARUSI ya kufana ilifanyika katika Kanisa la ... (C.P.K.) huko Kaloleni, Giriama baina ya Bw. ...